LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# KIAPO

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# KIAPO

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

1. MAANA YA KIAPO....10
2. AINA ZA VIAPO....10
2.1.Kiapo cha Maandishi....12
2.2.Nani Huapisha?....12
2.3.Mambo yanayopaswa kuwemo kwenye Hati ya Kiapo....13
3. MFANO WA KIAPO....15
4. HITIMISHO....20

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa Wanasheria walioshiriki katika uandaaji wa kijarida hiki. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususan, Wakili Godfrey Mpandikizi, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Bwana Rodrick Maro. Shkrani za pekee pia ziende kwa Wanasheria wa Kujitolea pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uweo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika endapo raia wangelikuwa na ufahahamu wa sheria. Ndiyo maana basi Kituo cha Sheria na Haki za Binadamui kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa ufahamu wa sheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni

lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu nawe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTANGULIZI

Jamii yetu imekuwa na uelewa mdogo sana kuhusiana na suala zima la kiapo jambo linalopelekea watu wengi kushindwa kesi zao mahakamani kutokana na kiapo kutofuata au kuzingatia utaratibu wa kisheria. Pia wanajamii wanapata usumbufu wa kufikia haki zao kutokana uelewa mdogo wa maana, sifa na taratibu za Kiapo.

Kijitabu hiki kimeandaliwa kwa lengo la kukuza uelewa kuhusu wa masuala mazima ya sheria ya kiapo, aina ya viapo na mambo muhimu yanayotakiwa kuwa kwenye kiapo. Mwishoni mwa kijitabu hiki kuna mfano wa kuandaa hati ya kiapo cha shauri lilopo mahakamani..

## 1. MAANA YA KIAPO

Kiapo ni maelezo anayotoa mtu ambayo mtu huyo anaamini kuwa ni sahihi na ya kweli. Kiapo kinaweza kutolewa kwa njia mbili, yaani:

i. Kwa njia ya matamshi (kwa njia ya mdomo);

ii. Kwa njia ya maandishi.

## 2. AINA ZA VIAPO

Kiapo cha matamshi hutolewa kwa mdomo na mtoaji kiapo hicho mbele ya kamishna wa viapo, akiapa na kukiri kwa imani yake, kuwa maelezo atakayotoa mbele yake ni sahihi na ya kweli. Viapo vya aina hii hutumika mara nyingi mahakamani pindi shahidi anapokuwa anatoa ushahidi kwenye kesi au shauri. Mathalan, Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6, Marejeo ya Mwaka 2002 ya sheria za Tanzania, imebainisha wazi kuwa kila shahidi katika kesi ya jinai au madai atatoa ushaidi wake mbele ya Mahakama kwa njia ya kiapo cha matamshi.

Lakini, kifungu cha 231 cha Sheria ya Mwenendo wa

Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Marejeo ya Mwaka 2002 kinampatia mshtakiwa, pale ambapo mahakama itaridhishwa na ushahidi wa upande wa mashtaka kwamba ana kesi ya kujibu, fursa ya kutoa ushahidi kwa kiapo au kwa kutotoa kiapo.
Kiapo cha maandishi hutolewa kwa maandishi na mtoaji kiapo mbele ya kamishna wa viapo, akiapa na kukiri kwa imani yake, kuwa maelezo aliyotoa kwa maandishi mbele yake ni sahihi na ya kweli. Kiapo cha maandishi: Viapo vya maandishi huwa vya aina tofauti tofauti kilingana na suala linalotakiwa kuthibitishwa kwa wakati huo. Kwa mfano, kuna kiapo kinachotolewa na mtoaji kwa ajili ya kuelezea sababu za kupeleka maombi ya kuomba nafuu fulani mahakamani, au kiapo cha kuthibitisha tarehe na mwaka wa kuzaliwa, au kiapo cha kuthibitisha upotevu au umiliki wa mali, nk.

Katika kijarida hiki, tutaongelea zaidi viapo vya maandishi, na hasa viapo vinachotolewa kwa ajili ya kuelezea sababu za kupeleka maombi ya kuomba nafuu fulani mahakamani. Kiapo hiki huambatana na maombi ya nafuu hiyo.

Hata hivyo, mahakama pamoja na kumruhusu mtoa kiapo kuwasilisha hati ya kiapo, mahakama hiyo hiyo inaweza kuamuru mtoa kiapo kufanyiwa mahojiano ya ana kwa ana kwa njia ya mdomo mbele ya mahakamani ili kuthibitisha ananchokieleza.

### 2.1. Kiapo cha Maandishi

Kama ilivyoelezewa hapo juu, kiapo cha maandishi hutolewa kwa maandishi na mtoa kiapo mbele ya kamishna wa viapo, akiapa na kukiri kwa imani yake, kuwa maelezo aliyotoa kwa maandishi mbele yake ni sahihi na ya kweli.

### 2.2. Nani Huapisha?

- Wakili;
- Jaji/Hakimu; na/au
- Mtu yeyote ambaye aliyekasimiwa kufanya kazi kwa Mujibu wa Sheria

## 2.3. Mambo yanayopaswa kuwemo kwenye Hati ya Kiapo

Ili kiapo kikamilike, yafuatayo ni mambo muhimu yanayotakiwa kuwemo katika maelezo ya kiapo:

1. Kichwa cha habari;
2. Jina la mtoa kiapo;
3. Maelezo yanayo mtambulisha mtoa kiapo, yakizingatia umri na msingi wa imani yake (Dini);
4. Maelezo ya mambo yanayothibitishwa na kiapo;
5. Kiapo chenyewe;
6. Eneo kiapo kilipotolewa
7. Saini ya mtoa kiapo;
8. Saini ya  Kamishna wa Viapo;
9. Mahali anapopatikana Kamishna wa Viapo; na
10. Wadhifa wa Kamishna wa Viapo (kama ni Jaji, Hakimu, au Wakili);
11. Tarehe;
12. Uthibitisho wa maelezo.

**ANGALIZO:**

Mtoa Kiapo ni lazima athibitishe ukweli na mambo aliyoandika au kusema kwa maandishi kwenye kiapo chake kama ni kweli na ameyafahamu vipi. Ni lazima ataje chanzo cha habari kilichompa maelezo iwapo maelezo hayo ameyapata kwa mtu mwingine; na kama ni yale yanayotokana na ufahamu wake mwenyewe, basi inampasa kuelezea hivyo. Pia ikumbukwe kwamba mambo ya ushahidi wa kusikia, kutaja vifungu vya sheria na kujadili ushahidi hayaruhusiwi ndani ya maelezo ya kiapo. Iwapo mambo hayo yataingizwa, basi kiapo hicho kitakuwa batili. Endapo itathibitika kiapo hicho ni batili kwa sababu ya kuingizwa kwa mambo yaliyotajwa hapo juu, basi hati hiyo ya kiapo itafutiliwa mbali na mahakama au kuamriwa kuandaa kiapo kingine au kuamuru kufutwa kwa aya inayokinzana na sharia ya viapo. Endapo Mahakama itaamuru kuondolewa kwa Hati ya Kiapo Mahakamani, inawezekana Mahakama ikamuamuru mtoa kiapo wa namna hiyo kulipa gharama zote za kesi au kutoa amri nyingine yoyote kadiri itakavyoona inafaa.

## 3. MFANO WA KIAPO

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
DAR-ES SALAAM KISUTU
SHAURI LA MADAI NA. ................/Mwaka..................
KISUMBE PAMBE..........................mtoa kiapo

DHIDI YA
MASHAURI JONGO.........................MDAIWA

KIAPO

Mimi, KISUMBE PAMBE, mtu mzima, mkristo, mwanaume na mkazi wa Dar es Salaam, mlalamikaji katika shauri hili, hivyo basi ninaelewa vya kutosha juu ya jambo ninalotaka kulitolea kiapo na hivyo naapa ifuatavyo:

1. Kwamba, mwaka 1999 nilifika katika kijiji cha Vijimbe na nikakabidhiwa

ardhi na Serikali ya Kijiji ili niitumie kuendesha kilimo cha mazao ya biashara;

2. Kwamba, shamba hilo lina ukubwa wa ekari ishirini, na nimepanda minazi na michugwa;
3. Kwamba, mwaka 2003 mdaiwa alikuja kulivamia shamba hilo akidai kwamba shamba hilo ni mali yake kwa kuwa aliachiwa kama sehemu ya urithi wake na marehemu babu yake mnamo mwaka 1980;
4. Kwamba, bila makubaliano yoyote yale na bila kupata idhini kutoka Serikali ya Kijiji, mdaiwa alianza kukata mazao shambani kwangu na kuanza kulima;
5. Kwamba, kutokana na kitendo hiki niliamua kilifikisha suala hili katika Mahakama yako tukufu, lakini hata hivyo mdaiwa bado anaendelea kulima kwa biidi na kupanda mazao katika shamba langu; na

6. Kwamba, iwapo maombi yangu niliyoyafikisha hapa mahakamani hayatakubaliwa ilikumzuia mdaiwa kuendelea na kilimo kwenye shamba lenye mgogoro, mimi mdai nitapata hasara isiyorekebishika.

UTHIBITISHO

Kwamba yote yaliyosemwa hapo juu kuanzia aya ya 1, 2, 3, 4, 5 na 6 ni kweli kutokana na ufahamu wangu mwenyewe.

| | |
|---|---|
| Kiapo kimetolewa Dar es Salaam<br>na KISUMBE PAMBE ambaye<br>Ametambulishwa kwangu na<br>____________________ ambaye<br>mimi mwenyewe ninamfahamu<br>mbele yangu leo hii<br>tarehe __________<br>mwezi __________<br>Mwaka__________ | ______________<br>Mtoa Kiapo |

**MBELE YANGU:**

JINA: ______________________________________

SAHIHI: ____________________________________

WADHIFA: ________________________________

ANUANI:_____________________________________

Imewasilishwa kwa ajili ya kuwekwa kwenye jalada leo hii

tarehe___________

mwezi___________

mwaka___________

____________________________________

KARANI WA MAHAKAMA

NAKALA ITUMWE KWA:

MASHAURI JONGO,

S. L. P. 48,

VIJIMBWENI,

DAR ES SALAAM.

IMETAYARISHWA NA:

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU,
IDARA YA MSAADA WA SHERIA KINONDONI,
MTAA WA ISERE,
S. L. P. 79633,
DAR E S SALAAM.

Huu ni mfano wa jinsi ya kuandaa kiapo kwa ajili ya kesi iliyo mahakamani inavyopaswa kutengenezwa. Kwa kawaida, hati ya kiapo huandikwa kwa lugha ya Kiingereza, kwa kuwa lugha rasmi ya kimahakama ni Kiingereza hususani kuanzia mahakama ya Wilaya mpaka Mahakama ya Rufaa.

# 4. HITIMISHO

Kutokana na maelezo yaliyotolewa kuhusu Kiapo, ni matarajio yetu kuwa ndugu msomaji utakuwa umenufaika vya kutosha. Kama tulivyoona kwenye kijarida hiki, hati ya kiapo itakubaliwa tu endapo mambo muhimu yaliyotajwa yatakuwa yamefuatwa. Endapo utashidwa kufuata hatua moja katika hayo basi, hati yako itatupiliwa mbali na mahakama na pia mahakama inaweza ikatoa amri kwa mtoa kiapo kulipa gharama ambazo upande mwingine utakuwa umepata. Kutokana na hayo, ni muhimu kufuata mfano wa hati ya kiapo uliotolewa katika kijarida hiki.

Pia ni ombi letu kwako kuwa kwa elimu uliyoipata katika kijarida hiki uitoe kwa watu wengine ili waweze kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kiapo, maana yake, kinavyotumiwa na bila kusahau mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuaandaa hati ya kiapo.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*